ELIMU INAYOZINGATIA UMAHIRI

TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 3 2026

GREDI YA 4

KISWAHILI LUGHA

MUDA: Dakika 40

JINA: _____NAMBARI YA AD: _____

SHULE: _____TAREHE: _____

MAAGIZO KWA WANAFUNZI

1. Karatasi hii ina **maswali 30 ya kuchagua jibu sahihi**.
2. **Jibu maswali yote.**
3. Kwa kila swali, chagua **jibu sahihi kati ya machaguo manne A, B, C na D**.
4. **Andika herufi pekee ya jibu sahihi** katika nafasi uliyopewa.
5. Soma kila swali kwa makini kabla ya kujibu.
6. **Usiandike jibu zaidi ya moja** kwa swali lolote.

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1–5.

Pendo na Neema wako kwenye uwanja wa shule yao wakati wa chakula cha mchana.

Pendo: Hujambo Neema? Leo unakula chakula gani?

Neema: Nala ugali na sukumawiki. Je, wewe unakula chakula gani?

Pendo: Nala wali, nyama na mboga. Chakula chako hakina chakula cha kujenga mwili. Hebu nikugawie nyama.

Neema: Asante sana, Pendo. Samahani, mimi huwa sili nyama.

1. Mazungumzo haya yaliendelea wakati gani?

A. Alasiri B. Adhuhuri C. Usiku D. Jioni

2. Neema angemjibu Pendo vipi baada ya kusalimiwa?

A. Sijambo B. Fiti C. Marahaba D. Niko poa

3. Neema alikuwa anakula chakula gani?

A. Wali, nyama na ugali
B. Wali, nyama na mboga
C. Ugali na sukumawiki
D. Mchuzi wa nyama

4. Nyama ni chakula cha aina gani?

A. Kuongeza nguvu
B. Kuongeza joto
C. Kuzuia magonjwa
D. Kujenga mwili

5. Kwa nini Neema alikataa nyama aliyopewa na Pendo?

A. Huwa hali nyama
B. Alikuwa na chakula chake
C. Alikuwa ameshiba
D. Pendo alikuwa adui yake